# Mifano ya Hatari za Mpango

## Vyanzo: maelezo yaliyojumuishwa kwenye hati hii yanatokana na kazi halisi iliyofanywa na shirika la FHI 360 pamoja na vyanzo kadhaa (vilivyobainishwa kwenye sehemu Nyenzo), ikijumuisha:

- Usimamizi wa Hatari kwa Kuzuia Mipango ya Vurugu: Mwongozo wa Watendaji
- Kubadilisha Misimamo Mikali yenye Vurugu: Mwongozo wa Mjenzi wa Amani
- Kuboresha Athari za Kuzuia Utayarishaji wa Ukatili wa Misimamo mikali: Zana ya kubuni, kufuatilia na kutathmini
- Mwongozo wa Utendakazi kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa inayolenga kukabiliana na ugaidi na shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu katika nchi zinazokua kiuchumi
- Mbinu Bunifu za Utayarishaji wa CVE: Maarifa na Masomo kutoka kwa Ofisi ya USAID ya Mikakati ya Mpito Mpango wa Kustahimili Jamii wa Lebanon (2014-2017)
- Mwongozo: Hatua 3 za Kufanya Kazi katika Maeneo Yasiyo na Usalama Uthabiti na Yaliyoathiriwa na Mgogoro (WFCs)

Hati hii hailengi kutarajia hatari ambazo zitapatikana kwenye mradi wako wa P/CVE au kutoa ushauri kuhusu hatari ambazo unapaswa kupangia kwenye mradi wako. Ni orodha ya mifano ya hatari ambazo watekelezaji au miradi mingine ya P/CVE imetambua na baadhi ya mwongozo wa kukadiria na kushughulikia hatari hizi. Hii si orodha kamili au inayopaswa kufaa kwa mradi wako. Ichukulie kama nyenzo ya kusaidia shirika lako kuanza kuwazia kuhusu makundi na aina za hatari ambazo zinaweza kuhusiana na mradi wako.

| HATARI GANI ILIYOPO? | SWALI MUHIMU LA KUKADIRIA NA KUSHUGHULIKIA HATARI |
|---|---|
| Hatua ya kushirikiana na wafadhili, hasa mashirika au serikali za nchi za nje, inaweza kuathiri jinsi wengine (serikali yako, jamii ya eneo au mashirika mengine ya eneo) wanavyochukulia shirika lako au jinsi wanavyoshirikiana na shirika lako. Hii inajumuisha:<br><br>Hii inajumuisha:<br>• Hatari kwa uaminifu na uhalali: shirika lako linaweza kuchukuliwa kama lenye mapendeleo au linalolenga kuendeleza maslahi ya nchi za nje.<br>• Hatari kwa usalama: shirika au wafanyakazi wako wanaweza kuwa chini ya uchunguzi wa kiwango cha juu na hata kusumbuliwa na serikali, mashirika ya usalama, makundi ya shughuli za VE au mashirika mengine. | • Wafadhili wako wanachukuliwaje na wadau mbalimbali?<br>• Je, kuna miradi mingine ambayo wafadhili wako wanatekeleza kwa sasa katika jamii/nchi yako? Ikiwa ndiyo, miradi hii inachukuliwaje?<br>• Hatua ya kukubali ufadhili kutoka kwa wafadhili fulani itaathiri aje uhusiano wa shirika lako na wadau mbalimbali?<br>• Je, kuna makundi ambayo yatasita au kukataa kushirikiana na shirika lako kwa sababu ya chanzo cha ufadhili?<br>• Je, hatua ya kushirikiana na mfadhili huyu itaathiri uwezo wa shirika lako wa kutekeleza baadhi ya shughuli kwa ufanisi na kwa usalama?<br>• Unawezaje kupanga na kuzungumzia kuhusu uhusiano wako na mfadhili huyu ili kushughulikia hatari hizi? |

| HATARI GANI ILIYOPO? | SWALI MUHIMU LA KUKADIRIA NA KUSHUGHULIKIA HATARI |
|---|---|
| Wahusika ambao mradi wako unashirikisha au kutoshirikisha wanaweza kusababisha hatari na kuleta athari mbaya kwa mpango wako, wanufaishwa/washiriki na kwa muktadha kwa ujumla zaidi. Hatari hizi zinaweza kujumuisha:<br>• Kutenga au kubagua zaidi watu, makundi au maeneo ambayo hayajachaguliwa<br>• Kushutumu watu, makundi au maeneo ambayo yamechaguliwa au kuyatia hatarini, ikijumuisha usalama wao.<br>• Kuimarisha au kuchangia vibaya katika miktadha ya utawala iliyopo na mitindo ya kutengwa katika jamii<br>KIDOKEZO: kwa maelezo zaidi kuhusu masuala yanayoweza kujitokeza kwa kushirikisha au kutoshirikisha vijana, angalia sehemu ya Ushirikishaji wa Vijana katika Mpango kwenye Moduli ya Kutekeleza [weka kiungo cha kuelekeza kwenye sehemu ya "Unawezaje kubuni mpango wako ili ufikie na kuchagua vijana?"] | • Mradi wako unashirikisha akina nani? Hatua ya kuwashirikisha inaathiri aje mradi wako, uhusiano wako na watu/makundi mengine na miktadha ya utawala katika jamii yako?<br>• Mradi wako haushirikishi akina nani? Hatua ya kutowashirikisha inaathiri aje mradi wako, uhusiano wako na watu/makundi mengine na miktadha ya utawala katika jamii yako?<br>• Utachaguaje watakaoshirikishwa katika mradi kama wanufaishwa au washirika?<br>• Tutawasilishaje mchakato wetu wa uteuzi na matokeo yake?<br>• Je, maelezo tunayokusanya kuhusu wanufaishwa wa mradi na washirika yanaweza kuwaweka hatarini? Je, tunashiriki na kulinda kwa njia gani maelezo tunayokusanya kuhusu jamii na watu binafsi katika jamii? Tunashiriki maelezo gani na washirika – kama vile wafadhili au mashirika ya serikali – na kuna hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na kushiriki maelezo haya?<br>• Ikiwa utashirikiana na/au kushirikisha serikali na mashirika yake, hatua ya kuyashirikisha itaathiri aje mradi wako, hasa ikiwa baadhi ya makundi yanachukulia kitendo au utendaji wa serikali kama tatizo?<br>• Ikiwa hutashirikiana na/au kushirikisha serikali na mashirika yake, hatua hiyo itaathiri matokeo na ufikiaji wa mradi wako? |
| Hatua ya kulenga mradi wako kwenye shughuli za P/CVE, hasa ikiwa huu ni mpango mpya katika shirika lako, inaweza kusababisha baadhi ya hatari, ikijumuisha:<br>• Inaweza kuathiri jinsi shirika lako linavyochukuliwa na wahusika wengine katika jamii yako na kuaminika kulingana na mitazamo yao. Kwa mfano, ikiwa mradi wa P/CVE utaonekana kama shughuli zinazolenga kikundi mahususi, huenda shirika lako likachukuliwa kwamba lina uhasama na kikundi hicho.<br>• Inaweza kudunisha au kuathiri kazi nyingine ambayo shirika lako limekuwa likifanya. Kwa mfano, ingawa kazi ya kukuza amani na ushirikishaji wa vijana inaweza kuchangia na kusaidia kubuni mpango wa P/CVE, huenda pia kukawa na wasiwasi unapozingatia zaidi eneo moja la mpango kuliko lingine, ikiwa mradi wako wa P/CVE unasababisha wahusika kusita kushirikiana nawe kwenye mipango ya aina nyingine. | • Hatua ya kushiriki katika miradi ya P/CVE inawezaje kuathiri uhusiano wako na wahusika na makundi tofauti katika jamii?<br>• Mipango yako ya uhamasishaji na ushirikishaji wa wadau inawezaje kusaidia katika kushughulikia hatari hizi?<br>• Je, hatua ya kuangazia kwa uwazi miradi ya P/CVE inaweza kuathiri uwezo wa shirika lako wa kufanya kazi na pengine usalama wa wale wanaohusika katika kazi yake? Ikiwa ndiyo:<br>  ‣ Je, inafaa kupanga mradi wako kwa njia tofauti? Ikiwa inafaa kufanya hivyo, utasawazishaje hali hiyo na hitaji la shirika lako la kuwa na uwazi na kuaminika?<br>• Je, kazi ya mradi wa P/CVE ni kipaumbele katika jamii yako na kwa shirika lako? Ikiwa ni kipaumbele, hali hiyo ilibainishwaje?<br>• Hatua yako ya kulenga mradi wa P/CVE inadunisha au kuathiri uwezo wako wa kutekeleza mipango ya aina nyingine? Ikiwa ndiyo:<br>  ‣ Ni athari gani inayoweza kujitokeza?<br>  ‣ Unaweza kufanya nini ili kushughulikia au kupunguza athari hii?<br>  ‣ Ni sababu gani ya msingi ya iliyofanya utoe kipaumbele kwa kazi ya mradi wa P/CVE? |

| HATARI GANI ILIYOPO? | SWALI MUHIMU LA KUKADIRIA NA KUSHUGHULIKIA HATARI |
| --- | --- |
| Miradi ya P/CVE mara nyingi hutekelezwa katika mazingira yasiyo thabiti au yasiyoweza kustahimili mabadiliko ya kimazingira hasa vitisho vya usalama vya kiwango cha juu, ikijumuisha kutoka kwa makundi ya dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu, makundi mengine ya vurugu au ya kihalifu au pengine vitendo vya serikali. Vitisho hivi vinaweza kuzuia mashirika kufikia maeneo au makundi fulani, kutekeleza shughuli zilizopo na vinaweza kuathiri usalama wa watu wanaohusika katika mradi. pia, ni muhimu kwa shirika kuendelea kukadiria hatari za usalama na kuchukua hatua zinazofaa ili kuzipunguza na kuzishughulikia. Hata hivyo, ni muhimu pia kwa shirika kuelewa na kushughulikia hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na mbinu zake za usalama na jinsi zinavyochukuliwa na wengine. Kwa mfano, hatua ya kuhamishia eneo la tukio nje ya eneo lisilo salama inaweza kufanya iwe vigumu kwa wadau muhimu kushiriki, au kuomba polisi wawepo katika tukio ili kuhakikisha usalama kunaweza kupandisha hadhi ya kiwango cha tukio hilo na kusababisha jamii kutokuwa huru tena kuhudhuria tukio hilo. | • Hali ya usalama iko vipi katika maeneo ambayo mradi wako utalenga?<br>• Je, makundi ya vurugu, ikijumuisha makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu yapo au yanatekeleza shughuli zake huko?<br>• Je, mradi utaweka wafanyakazi, washirika au wanufaishwa katika hatari kubwa?<br>• Ni nyenzo, michakato na mbinu gani ulizoweka ili kulinda wafanyakazi, washirika na wanufaishwa?<br>• Je, wafanyakazi wako wana mafunzo na maarifa yanayohitajika ili kushughulikia hatari za usalama iwapo zitajitokeza?<br>• Mbinu za usalama ulizoweka zinachukuliwa au zitachukuliwaje na wengine katika muktadha? Ni athari gani zinazoweza kujitokeza kwa kuchukua mbinu fulani?<br>• Kujenga uaminifu na uhusiano na washirika wa eneo na wadau kunaweza kuongeza kiwango cha usalama na ulinzi? |
| Kuna hatari zinazohusiana na matumizi ya nyenzo katika mradi wako wakati wa utekelezaji, na hizi zinahusiana hasa na mazingira ambapo mgogoro au makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu yanapatikana. Bila mbinu za udhibiti zinazofaa, fedha kutoka kwenye mradi wako zinaweza kuelekezwa kwa makundi haramu au ya uhalifu au zinaweza kuendeleza uchumi haramu au unaohusiana na mgogoro. | • Ni mbinu gani unazochukua ili kuhakikisha kwamba fedha hazitaelekezwa au kutumiwa kunufaisha makundi haramu au ya uhalifu?<br>• Nyenzo za mradi wako zinatoka wapi na ni nani anayenufaika kwa kuziuza/kuzikodisha? |
| Wanatimu wako pia wanaweza kuwa kigezo cha kusababisha au kushughulikia hatari.<br>• Watu unaoshirikisha kwenye timu yako ni muhimu; kwa mfano, ikiwa mradi wako unatekelezwa katika jamii yenye migawanyiko ya kikabila au kidini, ikiwa timu yako, hasa wafanyakazi wakuu na wanaofanya maamuzi kwenye timu hiyo, wanatoka katika mojawapo ya makundi haya, huenda mradi wako ukachukuliwa kuwa una mapendeleo. Pia, ikiwa baadhi ya wanatimu wako wanahusiana na kikundi fulani cha kisiasa, kuna hatari ambayo inaweza kutenga wanachama wanaopinga kikundi hicho.<br>• Ikiwa wanatimu hawana mafunzo na maarifa yanayohitajika ili kuelewa na kushughulikia miktadha ya mgogoro au kushirikisha watu ambao wanaunga mkono matendo ya vurugu au dhana za itikadi kali, hali hiyo inaweza kusababisha hatari ya kudunishwa kwa athari ya mradi wako na katika hali zingine, usalama wa wafanyakazi na washiriki. | • Je, taratibu zako za HR na uteuzi wa watu zinajumuisha kanuni za utofauti, ujumuishaji na uzingatiaji wa mgogoro ipasavyo?<br>• Historia ya wafanyakazi na misimamo yao kuhusu vigezo muhimu vinavyohusiana na mgogoro na shughuli za VE itaathiri aje mradi wako?<br>• Je, wafanyakazi wana mafunzo na maarifa yanayohitajika ili kutambua, kuelewa na kushughulikia miktadha ya mgogoro na wasiwasi katika kijamii?<br>• Wanatimu wako na uongozi wake wanazingatia na kuheshimu kanuni ya utofauti (kikabila, kidini, kijamii, kisiasa, n.k.) katika muktadha wako?<br>• Je, jamii na/au makundi mahususi katika jamii yanachukulia timu yako kuwa ina usawa?<br>• Je, historia au sifa za wanatimu wako (kabila/dini/misimamo ya kisiasa, jinsia, n.k.) zinaathiri aina ya shughuli ambazo wanaweza kushirikishwa ndani au mahali wanapoweza kwenda katika jamii? |

| HATARI GANI ILIYOPO? | SWALI MUHIMU LA KUKADIRIA NA KUSHUGHULIKIA HATARI |
| --- | --- |
| Ingawa hii kweli katika mradi wako wowote, kuondolewa na kufungwa kwa miradi ya P/CVE hasa kunaweza kusababisha wasiwasi na hatari ikiwa suala hilo halitashughulikiwa kwa umakini na kwa njia inayozingatia mgogoro uliopo. Miradi ya P/CVE mara nyingi hutekelezwa katika jamii ambazo hazina uwezo au zilizotengwa, na hatua ya kukomesha huduma au msaada unaotolewa inaweza kuzidisha matatizo na hali za kuvunjwa moyo, hasa ikiwa jamii haitarajii mradi huo kukoma au hailewi ni kwa nini msaada na huduma hizi zinabadilika au kukomeshwa. Kando na hayo, ufadhili wa mipango ya P/CVE hautegemeki na mara nyingi hutegemea mizunguko ya ufadhili na mipango iliyopewa kipaumbele na wafadhili wa kimataifa. Mara nyingi, ingawa kinachohitajika ili kushughulikia visababishi vya shughuli za VE ni miradi ya kudumu, shirika lako linaweza tu kupata ufadhili wa mfululizo wa miradi ya muda mfupi ambayo wakati mwingine ni vigumu kuibuni na kuitekeleza kama mpango mmoja. | • Ni athari gani mbaya zinazoweza kujitokeza kutokana na kukomeshwa kwa msaada au huduma zilizoanzishwa chini ya mradi wako?<br>• Je, timu yako ina mpango dhahiri wa kuondoa na kufunga shughuli na mradi wako?<br>• Ni vipengele gani ambavyo unaweza kujumuisha katika mpango wa shughuli zako ili kuhakikisha kwamba shughuli au matokeo yake yanadumu baada ya mradi kufungwa?<br>    ‣ Je, unaweza kushirikiana na wahusika wa eneo na kuendeleza hali yao ya kuwa sehemu ya umiliki wa miradi fulani ili waweze kuendeleza miradi hiyo baada ya mradi kukamilika?<br>• Ni mbinu gani unazoweza kuchukua ili kudhibiti matarajio ya washirika, wanufaishwa na jamii kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mradi?<br>    ‣ Unawezaje kuhakikisha kwamba huzui matarajio yasiyoweza kutimizwa wakati unashirikisha washirika, wanufaishwa na jamii ili kupata maoni na msaada wao kwa ajili ya mradi wako?<br>• Je, washirika wa mradi, wanufaishwa na jamii wanafahamu kwa jumla kwamba mradi unakamilika na wanaelewa ni kwa nini unakamilika?<br>    ‣ Ni mbinu gani (mikutano, mashauriano, nyenzo ya mawasiliano, n.k.) unazotumia ili kutayarisha washirika, wanufaishwa na jamii kwamba mradi unakaribia kukamilika au kukamilika kwa msaada wako kwa shughuli mahususi? |